MAPINDUZI
YA FIKRA
NA UCHUMI

DRAFT

# Azimio la Vijana la Kagera







# Maneno ya Mhe. Rais

## Kuhusu Azimio la Vijana la Kagera

Nimelipokea kwa furaha na kusoma Azimio la Vijana la Kagera linalosisitiza Mapinduzi ya Fikra na Uchumi. Nawapongeza sana vijana kwa kupaza sauti zenu kupitia Jukwaa la Fursa na kwa utashi wenu wenyewe kuja na Azimio la Vijana la Kagera.

Nawashukuru sana Kamati ya Fursa kwa kuitikia wito wangu nilioutoa siku ya tarehe 9 Novemba, 2017 nikiwa Bunazi wakati wa ziara yangu katika mkoa wa Kagera. Nilitoa wito kwa Kamati ya Fursa kuwafikia vijana na kuamsha vuguvugu la kuwajibika, kuzitafuta na kuchangamkia fursa zilizopo. Nafurahi kuwa wito ule uliwapa chachu ya kuandaa Mkutano wa Kilele wa Fursa mkoani Kagera ambao ulitoka na Azimio la Vijana la Kagera.

Nafarijika kuona vijana kupitia Azimio la Vijana la Kagera mmeamua kuchukua nafasi na dhima yenu katika kuiletea nchi yetu uhuru wa kiuchumi badala ya kubweteka na kulaumu. Nafarijika zaidi kuona utayari wenu katika kuunga mkono mapinduzi ya kiuchumi kwa kuanzia na mapinduzi ya fikra. Inatia moyo kwa sababu, vijana ni zaidi ya theluthi mbili ya Watanzania wote, hivyo, mkibadilika fikra na mkashiriki kuleta mapinduzi ya kiuchumi, nchi yetu itabadilika na safari yetu ya kufikia uchumi wa kati na uchumi wa viwanda itakuwa fupi zaidi kuliko inavyotarajiwa.

Kupitia Azimio la Vijana la Kagera, shabaha yenu na shabaha yetu sisi tulio katika Serikali zinaoana, na hivyo hatuna budi kushirikiana katika safari ya kuifikisha nchi yetu kwenye ukombozi wa kiuchumi, uchumi wa viwanda na uchumi wa kati. Napenda kuwahakikishia kuwa mimi na Serikali yangu tunaunga mkono juhudi zenu hizi na tuko tayari kushirikiana nanyi na kutekeleza wajibu wetu na kuwapa kila aina ya msaada mnaohitaji ili nanyi mtekeleze wajibu wenu.

***Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.***
***RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA***

# Maneno ya Mhe. Waziri

## Kuhusu Azimio la Vijana la Kagera

> Nawapongeza sana Kamati ya Kitaifa ya Fursa kwa kuandaa na kuridhia Azimio la Vijana la Kagera la Mapinduzi ya Fursa na Kiuchumi. Sisi katika Serikali tumefurahishwa na mwamko na uthubutu ulioonyeshwa na vijana kupitia Azimio la Vijana la Kagera.

Tumepokea mrejesho kuhusu changamoto ambazo vijana wanakabiliana nazo katika kusaka na kuchangamkia fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo yao. Hali kadhalika tumefaidika na maoni na mapendekezo yaliyotolewa na vijana na kuwekwa katika muktadha mzuri kupitia Azimio la Vijana la Kagera. Kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015-2020, Ibara ya 60, imetamka kuwa "Chama cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa vijana ambao ni kundi kubwa la nguvukazi.

Changamoto zinazowakabili ni pamoja na ukosefu wa ajira, elimu na maarifa ya kisasa katika uzalishaji mali, mitaji, biashara na ujasiriamali." Serikali ya Awamu ya Tano imeelekezwa kuzitafutia majawabu changamoto hizo na kuzitatua ili kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika kujenga nchi yetu kwa kadri ya vipawa na uwezo wao.

Nikiwa Waziri mwenye dhamana ya Vijana, napenda kuwahakikisha utayari wa Serikali kutatua changamoto zote zinazowakabili vijana na kufifisha ndoto zenu za kujiendeleza na mafanikio katika biashara, sanaa, ubunifu na michezo. Tunakaribisha na kuunga mkono Mapinduzi ya Fikra na Kiuchumi yaliyopendekezwa.

Tunaliona Azimio la Vijana la Kagera kuwa ni msaada mkubwa kwetu katika kutimiza azma yetu ya kuchochea maendeleo ya vijana. Tunaahidi ushirikiano wa Serikali na utayari wetu wa kuyafanyia kazi mapendekezo yatokanayo na Azimio la Vijana la Kagera.

***Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama (Mb.)***
***WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI NA VIJANA***



# Azimio la Vijana la Kagera

## ‘Mapinduzi ya Fikra na Uchumi’

Sisi vijana kutoka pande zote za Tanzania, tuliokusanyika mkoani Kagera katika Mkutano wa Kilele wa Kitaifa wa Fursa;

Tukijivunia kuwa sisi ndio kundi kubwa na nguvu kazi inayotegemewa na nchi yetu;

Tunaunga mkono Dira ya Taifa ya 2025 ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati;

Tunaitikia wito wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa kujenga Tanzania ya Viwanda;

Tunatambua wajibu wa kuijenga Tanzania ya Viwanda unaanza na sisi;

Tunaupokea kwa ujasiri wajibu wetu huu wa kihistoria, unaotutaka tujiongeze na kuongoza mapinduzi ya kiuchumi nchini;

Tukitambua utume wetu na wajibu wetu huu kwa Taifa; Kwa kauli moja, tunaitwaa dhima mikononi mwetu na kuazimia:

1. Kuleta Mapinduzi ya Fikra kwa kubadili mitazamo, fikra na dhana zinazoturudisha nyuma katika kujikomboa kiuchumi, ikiwemo utegemezi kwa Serikali, husda, kukatishana tamaa na kutoungana mkono;
2. Kuzikabili changamoto za kiuchumi zilizo mbele yetu, ikiwemo ushindani mkubwa katika soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, dunia ya utandawazi na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yajayo mbele yetu;
3. Kuibua fursa za kiuchumi ndani na nje kwa kuanzia sokoni, na kusaka na kuvuna fursa zilizo nje ya mipaka ya nchi yetu, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Duniani zitokanazo na Diplomasia ya Uchumi;
4. Kushikamana, kusaidiana na kuinuana kwa lengo la kuhakikisha kuwa kila mmoja, kwa kadri ya uwezo wake anapata nafasi ya kuifikia na kuitumia fursa anayoimudu inayoletwa na uchumi wa viwanda; na
5. Kuendeleza harakati za mabadiliko na mageuzi ya kiuchumi katika kuchochea maboresho katika mazingira ya kufanya biashara, kwa lengo la kuwezesha vijana kujikomboa na kumiliki uchumi wa nchi yetu.

***Kuanzia sasa,***
***Wajibu Kwanza Kabla ya Lawama!***
**-** *Bukoba, Desemba, 2017*

# Yaliyomo



**Maneno ya Mhe. Rais J. P. Magufuli kuhusu Azimio la Kagera**

Utangulizi
i. Azimio la Vijana la Kagera
ii. Chimbuko la Azimio la Vijana la Kagera
iii. Ushiriki na Ushirikishwaji katika Mchakato wa Azimio la Vijana la Kagera



**Maneno ya Mhe Waziri J. Mhagama kuhusu Azimio la Vijana la Kagera**

Malengo na Maudhui
i. Malengo ya Azimio la Vijana la Kagera
ii. Maudhui ya Azimio la Vijana la Kagera


Nguzo za Azimio la Vijana la Kagera



**Hitimisho; Shukrani kutoka kwa R. Mutahaba. Mweneyekiti Fursa**

Utekelezaji wa Azimio
i. Wajibu wa Vijana
ii. Wajibu wa Serikali
iii. Wajibu wa Wadau

Ufuatiliaji
i. Usimamizi wa Mpango wa Utekelezaji.



# 1

# Utangulizi

## Azimio la Vijana la Kagera ni Nini?

Azimio la Vijana la Kagera lilizaliwa Bukoba, Kagera katika Mkutano wa Kilele wa Fursa uliofanyika tarehe 16-17 Disemba, 2017, chini ya mwavuli wa Jukwaa la Fursa . Tofauti na maazimio mengine katika historia ya nchi yetu, Azimio la Vijana la Kagera si Azimio la Serikali wala Chama cha Siasa. Azimio la Vijana la Kagera linatokana na vijana na ni kwa ajili ya vijana wenyewe.

Msingi mkuu wa Azimio la Vijana la Kagera ni azma ya kuleta Mapinduzi ya Fikra na Uchumi katika nchi yetu, yatakayofungua fursa kwa vijana kushiriki moja kwa moja katika harakati za kujenga Tanzania ya Viwanda, na kuchangia jitihada za kuifikisha nchi yetu kwenye Uchumi wa Kati.

Sisi vijana ni zaidi ya theluthi mbili ya watu katika nchi yetu, na nguvu kazi pekee inayotegemewa kulivusha taifa letu kutoka tulipo kwenda kwenye uchumi wa kati.

Tumeridhika kuwa, hatuna budi kuchukua nafasi yetu na kujiandaa kikamilifu kukabiliana na changamoto zilizo mbele yetu. Tunapaswa kujiandaa kukabiliana na kumudu ushindani mkali katika soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Utandawazi, na zaidi, Mapinduzi ya 4 ya Viwanda yajayo, ambayo yamejikita katika ubunifu na matumizi ya teknolojia ya hali ya juu, inayotishia kuleta mabadiliko makubwa yenye kuathiri mifumo tuliyoizoea ya biashara, utendaji kazi na uzalishaji katika maofisi na viwanda, ikiwepo kutoweka kwa aina nyingi za ajira zilizopo leo.

Kupitia Azimio la Vijana la Kagera, vijana tunajitwika jukumu la kuchochea Mapinduzi ya Kiuchumi katika nchi yetu, ili kujiandaa kukabiliana na mabadiliko makubwa ya kidunia yajayo mbele yetu. Tumeazimia kuanzisha na kuendeleza vuguvugu na mageuzi yenye lengo la kubadili fikra, dhana na mitizamo ambayo imekuwa kikwazo kwa jitihada za vijana katika kufikia mafanikio katika nyanja za biashara na uchumi. Fikra na dhana hizi zimehusisha kwa kiasi kikubwa hali ya kutoshirikiana, kutosaidiana, kuhujumiana, kukata tamaa, kubezana na zaidi, kulaumu wengine hata kwa yale mambo yaliyo ndani ya uwezo wetu.

Ni dhahiri kuwa hatuwezi kwenda mbele kwa kuendelea kukumbatia fikra, dhana na hulka ambazo zimekuwa zikiturudisha nyuma. Tumaanini, wakati sasa umefika wa kubadili mitazamo yetu. Zama zimebadilika na hivyo hatuna budi vijana kubadilika. Tunafahamu kuwepo kwa changamoto zinazotukabili katika kufanikisha ndoto za kujikomboa kiuchumi ikiwemo upatikanaji wa mitaji, utitiri wa vibali, kodi, taasisi na sheria zinazojenga mazingira yasiyo rafiki kwa biashara.

Kupitia Jukwaa la Fursa, tumezunguka mikoa yote ya Tanzania na kujionea vijana, wake kwa waume wakichukua hatua moja mbele zaidi na kukataa kuwa mateka wa changamoto na vikwazo.  Tumekutana na vijana wenzetu ambao kwa ubunifu wao, kutokata tamaa kwao na kuwa na mtazamo chanya, amefanikiwa katika biashara na fani zao. Hawa ni kielelezo kuwa tukibadili mitazamo yetu na tunayoyatazama yatabadilika. Kupitia simulizi na uzoefu wao, tunaamini, tukitimiza wajibu wetu ipasavyo kwanza, kisha tukadai Serikali na wadau wengine kutimiza sehemu ya wajibu wao uliosalia, inawezekana kuleta Mapinduzi makubwa ya Kiuchumi katika uhai wetu.

Kwa ajili hiyo, Azimio la Vijana la Kagera ni wito wa uwajibikaji. Azimio linasisitiza vijana kutanguliza na kutimiza wajibu wao kwanza kabla ya kutoa lawama. Azimio linatutaka vijana kujiongeza na kujiongoza kwa kuwajibika na kuwajibishana. Kupitia Azimio hili, tumeazimia kutimiza wajibu wetu, kwa kufanya yale yaliyo katika uwezo wetu kwanza, kabla ya kudai uwajibikaji wa wadau na mamlaka nyingine.

Kesho yetu na vizazi vyetu, inategemea sana utayari wetu wa leo kuleta Mapinduzi ya Fikra na Uchumi. Wajibu huu unatuangukia sisi, ni wetu na hakuna badala yetu. Mtaji wetu ni wingi wetu, wakati pia uko upande wetu na sasa tunayo dira yetu, Azimio la Vijana la Kagera.



# Chimbuko la Azimio la Vijana la Kagera

Azimio la Vijana la Kagera ni matokeo ya miaka 5 ya Kongamano la Fursa ambalo limekuwa likifanyika nchini. Lengo la makombamano hayo lilikuwa ni kushirikiana na vijana katika kuzitafutia majawabu changamoto zinazowakabili na kuwarudisha nyuma katika jitihada zao za kujikomboa kiuchumi na kujiletea maendeleo.



Kwa miaka 5 mfululizo, Kongamano la Fursa limefanyika katika mikoa yote nchini likiibua fursa mbalimbali zilizoko katika mikoa na kitaifa, na kuhamasishana kuzichangamkia fursa hizo. Maudhui ya makongamano hayo yalikuwa yafuatayo:

- 2013: Jitathmini, Jiamini, Jiongeze
- 2014: Kamata Fursa twenzetu
- 2015: Fursa 10
- 2016: Ongeza Thamani
- 2017: Anzia Sokoni

Katika miaka 4 ya uhai wake, Kongamano la Fursa halikuwahi kufanya Mkutano wa Kilele wala kutoka na Azimio. Hivyo, Azimio la Vijana la Kagera ni muitikio mahsusi wa wito wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alioutoa tarehe 8 Novemba 2017 akiwa Bunazi mkoani Kagera.

Katika wito wake, Mheshimiwa Rais aliwaomba waandaaji wa Kongamano la Fursa kusaidia kuhamasisha vijana kushiriki katika Mapinduzi ya Kiuchumi katika kufanikisha azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda na kuifikisha nchi yetu kwenye uchumi wa kati. Kufuatia wito huo, na kwa kuzingatia kuwa wito huo aliutolea akiwa mkoani Kagera, iliamuliwa kuwa Kongamano la Kwanza la Kitaifa la Fursa lifanyike mkoani Kagera na ndipo lilipozaliwa Azimio la Vijana la Kagera.

# Ushiriki na Ushirikishwaji

Azimio la Vijana la Kagera ni matokeo ya ushiriki na ushirikishwaji mpana wa vijana na wadau mbalimbali kutoka nyanja mbalimbali kote nchini kupitia Kongamano la Fursa.

Katika kipindi cha miaka 5, kupitia makongamano 90, Kongamano la Fursa limeweza kuwafikia ana kwa ana vijana wajasiriamali wapatao 250,000 na vijana wengine milioni 3 kupitia televisheni, radio na mitandao ya jamii kila mwaka. Katika historia na uhai wa nchi yetu, hapajawahi kutokea vuguvugu la vijana wenyewe lenye ushiriki na uwakilishi mpana kama Kongamano la Fursa. Hili linafanya Azimio la Vijana la Kagera kuwa ni Azimio la Watu.



2

# Malengo na Maudhui

## Malengo ya Azimio la Vijana la Kagera

Lengo kuu la Azimio la Vijana la Kagera ni kuchochea Mapinduzi ya Fikra na Uchumi. Kufikiwa kwa lengo hilo kutategemea na namna vijana tutakavyoweza kutwaa fursa za kiuchumi na kutekeleza wajibu na mchango wetu katika jitihada za Serikali za kujenga Tanzania ya Viwanda na Uchumi wa Kati.

Malengo mahususi ya Azimio la Vijana la Kagera ni pamoja na:

i. Kuhamasisha ushiriki wa vijana katika shughuli halali za kijamii na kiuchumi katika maeneo walipo;

ii. Kushawishi mabadiliko ya fikra, dhana na mitazamo inayozuia vijana kuchangamkia na kutumia fursa zilizopo;

iii. Kupashana habari na taarifa juu ya fursa zilizopo na zijazo ndani na nje ya nchi ili kuandaa mazingira na utayari wa kunufaika nazo;

iv. Kushirikiana kwa kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kujengeana uwezo ili kuchochea ukuaji wa biashara na vipaji; na

v. Kuunganisha sauti kudai mageuzi makubwa katika uchumi wetu yenye lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa vijana ikiwemo uwepo wa miundombinu wezeshi kwa biashara, urahisi wa kupatikana kwa mitaji, unafuu na urahisi wa kulipa kodi, ada na tozo, na uwepo wa sera na sheria rafiki kwa vijana hususani wajasiriamali wa wadogo na kati.



## Maudhui ya Azimio la Vijana la Kagera

Maudhui ya Azimio la Vijana la Kagera yanajumuisha dhana tatu muhimu zenye kuchagiza Mapinduzi ya Fikra na Uchumi. Dhana hizo ni zifuatayo:

### i. Dhana ya Kuanzia Sokoni

Vijana wa leo tuna fursa nyingi na kubwa kuliko vijana waliopata kuwapo kabla yetu katika historia ya nchi yetu. Uwepo wa miundombinu ya barabara, mawasiliano na teknolojia kumepanua na kufungua fursa nyingi za kiuchumi. Dhana ya kuanzia sokoni inahimiza kuacha kufanya biashara kwa mazoea na badala yake kuenzi matumizi mazuri ya utafiti na taarifa juu ya hali ya soko na mahitaji kabla ya uamuzi wa kuanzisha shughuli ya kipato na biashara. Matumizi mazuri ya teknolojia ya habari na mawasiliano ni nyenzo muhimu ya kupata taarifa za soko na kuyahudumia mahitaji hayo kwa ubunifu na kujitofautisha. Popote ulipo fursa zipo. Jawabu ni kuanzia sokoni na kuwa mbunifu.

### ii. Dhana ya Ubunifu

Moja ya sababu zinazoturudisha nyuma kiuchumi ni kukumbatia hulka inayofanana na 'mdudu kaa' aishie baharini ya kumvuta chini aliye juu badala ya kusaidiana wote kupanda juu. Tabia za kuigana biashara, kuhujumiana na kuhusidiana katika biashara zinaminya fursa badala ya kuzitanua. Tunaongeza njia kwa kufyeka vichaka na mapori mapya si kupita njia ile ile aliyopita mwenzetu. Dhana ya Ubunifu inasisitiza katika kubuni mbinu na bidhaa mpya kwa lengo la kuongeza urefu wa mnyororo wa thamani wa bidhaa au huduma ya mwingine ambaye ametangulia sokoni. Tuwezeshane, Tusikwamishane.

### iii. Dhana ya Ujasiria-jamii

Changamoto na matatizo ya jamii inayotuzunguka ni fursa. Maendeleo makubwa yaliyotokea duniani kutokana na utandawazi yamekuja na changamoto nyingi. Kumekuwepo na mahitaji makubwa ya majawabu na suluhisho ya changamoto. Matokeo yake, majawabu na suluhisho sasa ni bidhaa. Haja hii imezaa wajasiria-jamii ambao shughuli zao za ridhiki na kipato zinatokana na kutatua changamoto zilizopo kwenye jamii ikiwemo usafi wa mazingira, malezi ya watoto, ukusanyaji, uhifadhi na uharibuji na uchakataji wa takataka, usafi na utunzaji wa mazingira, usambazaji wa maji safi na salama, vituo vya shule za awali za watoto na utoaji wa huduma muhimu za kijamii. Nyingi ya shughuli hizi zilikuwa huduma za bure na kujitolea huko nyuma, sasa ni bidhaa, zinauzwa na kununulika.



# 3

# Nguzo za Azimio



Azimio la Vijana la Kagera limesimama juu ya nguzo ambazo ndio muhimili wa Azimio lenyewe. Nguzo hizi ndio msingi unaowezesha kutekelezwa kwa Azimio hili. Nguzo hizi nne ni zifuatazo:

## i. Nguvu Kazi (Human Capital)

Dunia inashuhudia mabadiliko makubwa na ya haraka pengine kuliko wakati mwingine wowote katika maisha ya binadamu. Msingi mkubwa katika mabadiliko haya ni kasi ya matumizi na ukuaji wa tekinolojia. Hata hivyo, nchi yetu ina changamoto kubwa ya ukosefu na ufanisi wa nguvu kazi. Ukosefu wa Nguvu Kazi yenye Uweledi zinaathiri uwezo wa vijana na taifa kwa ujumla kumudu ushindani wa kibiashara na soko la ajira ndani nan je ya nchi. Tunaamini kuwa ili kuzikabili changamoto hizi, mageuzi makubwa ya mfumo wa elimu yanahitajika haraka kuwezesha upatikanaji wa nguvu kazi inayoendana na mahitaji ya dunia ya leo. Sambamba na hilo, tunaamini kuwa lazima kama taifa tufanye uwekezaji wa kutosha kwenye Nyanja za sayansi, utafiti, hisabati, ubunifu na uvumbuzi ili kuwandaa vijana kuzikabili changamoto za kiuchumi na kijamii kwenye karne ya ishirini na moja.

## ii. Uwezo (Capacity Development)

Tunaamini kuwa, dhamira, ari na nguvu pekee havitoshi kutufikisha kwenye lengo letu la Mapinduzi ya Fikra na Uchumi kuelekea uchumi wa kati na uchumi wa viwanda. Ili tufike kwa uhakika katika uchumi wa kati na viwanda hatuna budi kujenga na kuendeleza uwezo kwa upande wa stadi na maarifa, ili kuweza kumudu ushindani na kung'aa katika uchumi wa kati na viwanda. Tunalazimika kujinoa na kuwekeza katika maarifa mapya na mbinu mpya katika ubunifu, uzalishaji na ushindani sokoni. Sasa tunashiriki soko moja la dunia nzima, tusipoamua kujijengea uwezo na kushindana kwa mtazamo wa kidunia, hata sehemu yetu ndogo ya soko itatwaliwa na wengine, na tutabaki kuwa walaji na si wazalishaji.



### iii. Fikra Mpya (Mindset Change)

Dunia imebadilika na zama zimebadilika. Hakuna budi na mitazamo yetu kubadilika. Tulizoea kusema kuwa nchi yetu ni ya wakulima na wafanyakazi. Leo, Tanzania si tena nchi ya wakulima na wafanyakazi, bali ni nchi pia ya wafanyabiashara, wabunifu, wasanii, wavumbuzi na wanamichezo. Hali kadhalika, mitazamo tuliyonayo juu ya fursa, ajira, ujira na dhana ya mtu kufanikiwa kwa ujumla ndio minyororo yetu inayofunga uwezo wa kufanya vizuri kuliko tunavyofanya sasa. Ni wazi kuwa hatuwezi kutoka hapa tulipo kwa kukumbatia fikra, hulka, mitazamo na visingizio vile vile tunavyotumia kukwepa wajibu wetu. Ili twende mbele, hatuna budi kuachana na tabia




za kulalamika, kubeza, kulaumu, kutamani mafanikio ya haraka, kutegemea miujiza na kubagua kazi. Ni wakati sasa wa kuwa na fikra na mitazamo chanya, kuona fursa kwenye vikwazo, funzo kwenye kukosea na matumaini kwenye kukata tamaa.

### iv. Taasisi Imara (Strong Institutions)

Mafanikio yetu mbali na jitihada zetu wenyewe, yanategemea pia mchango wa taasisi zetu zikiwemo taasisi za malezi na taasisi za Serikali. Taasisi za malezi ndio zenye jukumu la kutulea na kutuandaa vijana kutwaa wajibu wetu na kutujenga kukabiliana na maisha. Taasisi kama familia, shule, dini zina mchango wa pekee na zinapaswa kutimiza wajibu wao kikamilifu. Kwa upande mwingine, taasisi za Serikali zina wajibu wa kuwezesha vijana kutimiza ndoto zetu na wajibu wetu kwa taifa. Tunadai mabadiliko katika uendeshaji wa taasisi za Serikali ili ziwe wezeshi na sio kikwazo. Tunataka Taasisi zinazofungua milango badala ya kujenga kuta, Taasisi zinazotufuata badala ya kutukimbia, Taasisi ambazo kipaumbele chake ni kutoa huduma badala ya kuadhibu na Taasisi zinazojivunia kulea biashara badala ya kufurahia kuzifungia.

### v. Sera Wezeshi (Enabling Environment)

Sera ni matokeo ya maamuzi ambayo huzaa sheria, taasisi, hutoa mwelekeo na huweka



miongozo mbalimbali, inayoathiri mwenendo wa uchumi kwa ujumla, biashara na soko. Tunatambua, sera huumba fursa na sera huua fursa. Kwa ajili hiyo, Mapinduzi ya Fikra na Uchumi hayawezi kukamilika bila kuwapo mabadiliko ya sera ambazo ni kikwazo kwa ustawi wa vijana katika sekta za biashara, sanaa, ubunifu, uvumbuzi na michezo.

Hatuna budi kuunganisha nguvu zetu kudai kuwepo kwa mazingira mazuri ya kisera, sera zinazonyumbulika kukidhi mahitaji ya vijana katika makundi na muktadha tofauti, na muhimu zaidi, sera wezeshi zinazotoa urahisi wa vijana kuanzisha biashara, kuifikia mitaji, kuondoa vikwazo kwa biashara ndogo na kati kukua, na kurahisisha ufanyaji biashara ya ndani na biashara ya nje.



# 4

# Utekelezaji wa Azimio

Uhai wa Azimio lolote ni kutekelezwa. Tofauti ya Azimio la Vijana la Kagera ikilinganishwa na maazimio mengine nchini kwetu ni kuwa, Azimio hili pamoja na kuwa ni la kitaifa, si Azimio lililotokana na Serikali au Chama cha Siasa. Azimio la Vijana la Kagera ni letu, kutoka kwetu kwa ajili yetu.

Ndio sababu, Azimio la Vijana la Kagera linatutaka vijana tutangulize wajibu wetu kwanza kabla ya kurusha lawama kwa yoyote. Hivyo, tunaweza kusema bila kupepesa macho kuwa wajibu wa kwanza wa kulitekeleza Azimio la Vijana la Kagera ni wetu sisi wenyewe.

Hata hivyo, hii haiondoi ukweli na uhalisia kuwa, mafaniko ya utekelezaji wa Azimio la Vijana la Kagera yanategemea pia, utekelezaji wa Serikali na wadau wengine, kwa yale mambo yanayoangukia katika wajibu wao. Tutatekeleza wajibu wetu kwanza, kisha tutaomba, tutashawishi na ikilazimika tutadai watekeleze wajibu wao. Wajibu na majukumu ya utekelezaji wa Azimio la Vijana la Kagera yanafafanuliwa kama ifuatavyo:

## i. Wajibu wa Vijana

a. Kusaka na kuchangamkia fursa na maarifa kwa kadri ya uwezo wetu, na kutumia fursa na maarifa hayo kufanikiwa na kuwezesha vijana wengine, na kuhakikisha hatumuachi kijana yoyote nyuma yetu katika safari ya Tanzania ya Uchumi wa Kati na Viwanda;

b. Kutumia vizuri fursa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) kwa kubadilisha matumizi kutoka kuwa nyenzo ya kueneza chuki, husda na umbeya kama ilivyo sasa, na kuitumia kuchochea mabadiliko ya fikra, kupashana na kubadilishana taarifa juu ya fursa zilizopo, na mbinu na maarifa ya kuzifikia na kuzitumia. Nyezo hii tuitumie kupunguza gharama za uendeshaji biashara, kufanya mapinduzi ya uzalishaji, kuongeza ufanisi na kulikabili soko la dunia pasipo kujali mipaka ya kiutawala.

c. Kutanua na kurefusha mnyororo wa fursa kwa kuondokana na tabia ya kuigana na kuhujumiana, na badala yake kujenga utamaduni wa kushirikiana kwa kuungishana, kushindana bila kushindwana na kwenda hatua moja zaidi ya pale ambapo ubunifu, bidhaa au huduma ya mwenzetu inapoishia;

d. Kutii na kufuata sheria na taratibu zilizopo ikiwa ni pamoja na kujishughulisha na kujiingiza katika shughuli halali za kujipatia kipato na kiuchumi zisizo na madhara kwa jamii na nchi yetu na kuwa mfano wa kuigwa kwa vizazi vijavyo; na

e. Kulitangaza Azimio la Vijana la Kagera na kulitumia kuunganisha nguvu za vijana wote kudai mageuzi ya kiuchumi, na mazingira mazuri ya kisera, kisheria na kitaasisi yatakayowezesha vijana kushiriki kikamilifu, katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na hatimaye uchumi wa kati. Kulitumia Azimio hili kama rejea ya mijadala yetu ya kijamii na kitaifa kuhusu masuala ya kiuchumi, kuamsha ari na kutatua changamoto za vijana.

## ii. Wajibu wa Serikali

a. Kuweka mazingira wezeshi ya kisera, kisheria na kitaasisi yanayochochea ustawi wa vijana, hifadhi ya jamii, na kuwawezesha kufikia kilele cha ndoto zao, na ukomo wa uwezo, vipaji na vipawa vyao katika nyanja zote iwe ni katika uongozi, biashara, uvumbuzi, ubunifu, sanaa na michezo;

b. Kuwatujengea vijana uwezo kwa kutupatia stadi muhimu za kiuongozi, biashara na kitaasisi ili tuweze kuendana na kasi ya mabadiliko ya dunia, kumudu ushindani katika Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutuandaa kikamilifu kutoachwa nyuma na kukabiliana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yajayo mbele yetu;

c. Kuhakikisha upatikanaji wa taarifa kuhusu fursa za elimu, uendelezaji vipaji, biashara na uchumi na zipatikanazo nchini na zile za nje zitokanazo na mkakati wa Diplomasia ya Uchumi;

d. Kuchochea upatikanaji wa mitaji kwa vijana, hususan biashara ndogo na kati, kwa kuweka sera zinazoshawishi taasisi za fedha za umma na sekta binafsi kukopesha vijana kwa masharti nafuu, ikiwemo kuunganisha mifuko mbalimbali ya uwezeshaji iliyopo chini ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi la Taifa (NEEC) na kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Vijana, Biashara Ndogo na Kati; na

e. Kufanyia mapitio sera ya manunuzi na Sheria ya Manunuzi ya Umma Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 na kuelekeza walau asilimia 30 ya manunuzi ya bidhaa na huduma yanayofanywa na Serikali Kuu, Idara na Taasisi zake na Serikali za Mitaa yatokane na biashara ndogo na kati zinazomilikiwa na vijana.

## iii. Wajibu wa Wadau

a. Kuunga mkono Azimio la Vijana la Kagera kwa kuwekeza kubadili mtazamo wa kuwachukulia vijana kama soko na badala yake kuwekeza kuwawezesha kwa kuwachukulia kuwa ni hazina ya sekta binafsi ya leo na kesho ya nchi yetu;

b. Kuwekeza katika sekta ya uvumbuzi, ubunifu, sanaa na michezo ili kuendeleza na kuvuna mtaji wa vipaji miongoni mwa vijana, na kuwawezesha vijana kutafsiri vipaji vyao kutoka kuwa majaliwa na kuwa fursa na biashara;

c. Kutenga na kutoa fursa ya mafunzo ya vitendo kwa vijana wabunifu, wasaniii na wafanyabiashara ndogo na kati ili kuwajengea uwezo, ujuzi na maarifa ya kukuza shughuli na biashara zao kutoka zilipo na kuwa kubwa;

d. Kutenga na kufanya manunuzi yasiyopungua walau asilimia 30 ya bidhaa na huduma kutoka kwa wazalishaji, watoa huduma na wagavi vijana, ikiwa ni sehemu ya sera ya Uwajibikaji wa Makapuni kwa Jamii; na

e. Kuandaa na kushiriki katika Tuzo ya Azimio la Vijana la Kagera itakayotolewa kwa makampuni na taasisi zenye kutoa mchango mkubwa katika kusaidia utekelezwaji wa Azimio la Vijana la Kagera.

## Usimamizi wa Mpango wa Utekelezaji

Azimio la Vijana la Kagera litatekelezwa na wadau wote chini ya uratibu wa Kamati ya Kitaifa ya Fursa itakayokuwa na jukumu la kuandaa, kusimamia, kufuatilia na kuratibu Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Azimio la Vijana la Kagera. Utekelezaji wa Azimio la Vijana la Kagera na Mkakati wake vitafanyiwa tathmini kila mwaka kupitia Jukwaa la Fursa katika ngazi za mikoa na Taifa.
















# 5 Hitimisho

Vijana wa Tanzania tunacho kila tunachohitaji kututoa hapa tulipo kutufikisha kwenye maisha yaliyo bora zaidi, kwenye Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati. Tunachohitaji ni kukusanya pamoja nia, ari, uthubutu wetu chini ya Azimio la Vijana la Kagera, kwa kufanikisha Mapinduzi ya Fikra na Kiuchumi katika nchi yetu.

> ***Tunao wajibu mabegani mwetu wa kukabidhi vizazi baada yetu, Tanzania iliyo bora zaidi kuliko ile tunayoipokea kutoka kwa vizazi kabla yetu. Wajibu huu ni wetu, hakuna badala yetu.***

***Wajibu Kwanza. Kabla ya Lawama!***

# 6

# Shukrani

Simulizi ya miaka mitano ya fursa kufikia Azimio la Vijana la Kagera, sio tu ina mengi ya kusimulia na kujifunza, ila ina wengi wa kusimulia nao.

Kwanza, tunawashukuru vijana wote waliojitokeza kwa wingi katika mikutano ya Fursa na kuelezea uzoefu wao na changamoto zao. Tunawashukuru kwa utayari wao waliotuonyesha wa kukaribisha mapinduzi ya fursa na ari yao ya kuleta mapinduzi ya kiuchumi. Tumeuona ubunifu, uthubutu na utayari wao wa kuleta Mapinduzi ya Fikra na Uchumi katika nchi yetu. Uzoefu waliotupatia, changamoto walizoziainisha na mapendekezo waliyoyatoa ndio vilivyowezesha kuandaliwa na kukamilika kwa Azimio la Vijana la Kagera. Itoshe kusema, Azimio la Vijana la Kagera ni lao wenyewe, kwao wenyewe na kwa ajili yao wenyewe.

Pili, tunahadithi nyingi za kusimulia za viongozi wetu kuanzia ngazi ya serikali za mitaa hadi serikali kuu nchi nzima. Wameshirikiana nasi kuwaleta vijana pamoja, kutuhakikishia usalama na amani kwenye mikutano yetu na kuitikia wito kila tulipowaita kuongea na vijana wenu, na hata kutekelezea mengi ya mahitaji yao ya kimageuzi kibiashara waliyoyapendekeza katika mikutano ya Fursa. Kwa upekee kabisa tunawiwa na wajibu wa kuwashukuru Marais wote wa awamu mbili za maisha ya miaka mitano ya Fursa; Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliyezindua Semina za Fursa mwaka 2014 na Rais John Pombe Magufuli aliyetupa changamoto ya kuwa na Mkutano wa Kilele wa Fursa akiwa ziarani mkoa wa Kagera na hivyo kuzaliwa kwa Azimio la Vijana la Kagera.

Mwisho, ni shukrani kwa taasisi zote washirika wa Fursa: Shirika la Umoja wa Mataifa (UN), Benki ya Letshego, Wizara ya Afya kupitia kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira (Usichukulie Poa Nyumba ni Choo) na Clouds Media Group waliotoa michango yao ya kitaalamu, kifedha na kiuwezeshaji katika kufanikisha Mkutano wa kilele cha Fursa unafanyika Mkoani Kagera na kuwezesha ujumbe wa Fursa kuwafikia vijana kokote walipo. Tungeweza kuwataja, lakini ukurasa huu hautoshi kubeba uzito wa shukrani zetu kwa kila mmoja wenu mmoja mmoja. Kwa pamoja tunasema asanteni sana.

Nina imani thabiti kuwa Azimio hili litaleta mabadiliko makubwa kwenye maisha ya vijana wa Tanzania, na ninawashukuru kwa kulipokea na utayari wenu wa kuliishi. Huo ndio mwisho wa kufurahisha tunaoutarajia kwenye simulizi hii.

***Ruge Mutahaba***
***MWENYEKITI, FURSA***




TATU
Mzuka!
USICHUKULIE POA
NYUMBA
NI CHOO






Azimio la
Kagera






Kagera
Clouds
TATU
Mzuka!



UHURU NA UMOJA

Azimio la Kagera
Mapinduzi ya Fikra na Uchumi

fursa Consultancy
Complex Problem Solving